**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**WILAYA YA UKEREWE**

**MTIHANI WA KIDATO CHA KWANZA**
**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**MUDA SAA 2:30** **MWAKA: 2025**

---

MAELEKEZO

1. Mtihani huu unasehemu A,B na C zenye jumla ya maswali kumi **(10)**
2. Jibu maswali yote
3. Andika jina lako katika kila ukurasa wa karatasi yako ya kujibia
4. .Majibu yote yaandikwe kwa usafi na kwa uwekevu.

## SEHEMU A (Alama 15)

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika kipengele (i) mpaka cha (x) kisha andika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya karatasi ya mtihani uliyopewa

i. Somo la Historia ya Tanzania na Maadili linajumuisha dhana kuu ngapi?
   a) Moja
   b) Mbili
   c) Tatu
   d) Nne

ii. Historia inahusu mambo gani?
   a) Mambo ya sasa
   b) Mambo yaliyopita
   c) Mambo yajayo
   d) Mambo ya kubuni

iii. Ni kwa nini ni muhimu kujua historia yetu?
   a) Ili kuishi maisha ya anasa
   b) Ili kusafiri nchi za nje
   c) Ili kuelewa tulikotoka, tulipo, na tunakokwenda
   d) Ili kuwa maarufu

iv. Mabadiliko gani yamekuwa yakizingatiwa katika historia ya Tanzania?
   a) Mabadiliko ya hali ya hewa
   b) Mabadiliko ya teknolojia pekee

c) Mabadiliko ya kijamii, kisiasa, na kiuchumi
d) Mabadiliko ya michezo

v. Maadili ni nini?
a) Miongozo inayotawala tabia ya mtu na jamii
b) Sheria za nchi
c) Tamaduni za nchi za nje
d) Mambo ya kidini tu

vi. Maadili yana umuhimu gani kwa taifa?
a) Kujenga majivuno
b) Kukuza uhasama
c) Kutambulisha utu wetu, kujenga heshima, na kuleta maendeleo
d) Kuleta machafuko

vii. Somo la Historia ya Tanzania na Maadili linatusaidiaje?
a) Kujenga chuki
b) Kuelewa mila, desturi, na maadili ya jamii za Tanzania
c) Kuiga tamaduni za kigeni
d) Kuacha mila zetu

viii. Ni nini umuhimu wa somo la Historia ya Tanzania na Maadili?
a) Kujifunza lugha za kigeni
b) Kujenga moyo wa kuipenda, kuilinda, na kuiheshimu nchi yetu
c) Kusafiri duniani
d) Kuwa na mali nyingi

ix. Somo la Historia ya Tanzania na Maadili linahusiana na masomo gani mengine?
a) Jiografia, Hisabati, Kiswahili, Kiingereza, Chakula na Lishe, Sanaa na Michezo, Muziki, na Kilimo
b) Fizikia na Kemia pekee
c) Biashara na Ujasiriamali pekee
d) Ufundi na Teknolojia pekee

x. Ni kwa nini maadili ni muhimu katika jamii?
a) Huleta fujo
b) Huleta ubaguzi
c) Huleta amani, upendo, na maelewano
d) Huleta vita

2. Oanisha **SAFU A** kwa kutoa jibu sahihi kutoka katika **SAFU B** kisha andika herufi ya jibu sahihi katika visanduku chini yake.

| Orodha A | Orodha B |
|---|---|

| | |
|---|---|
| i) Kundi rika la vijana wa kimasai wenye wajibu wa kuhakikisha ulinzi na usalama wa jamii zao.<br>ii) Kiongozi wa juu zaida wa kisiasa wa kabila la wamasai.<br>iii) Kundi muhimu katika jamii ya kimasai lenye watu wenye umri kuanzia miaka 40 na kuendelea lenye majukumu ya kufanya maamuzi na kusuluhisha migogoro.<br>iv) Uhusika zaidi na shughuli za nyumbani ukamuaji wa maziwa na ujenzi wa nyumba.<br>v) Majukumu yao karibu na yalipo makazi ya jamii zao. | A.Ol aiguanani<br>B.Wazee<br>C.Wabarabaigi<br>D.Laibon<br>E.Watoto wa miaka 0-8<br>F.Marani<br>G. Watoto wa miaka 8-18<br>H.Wanilo<br>I.Wanawake |

**SEHEMU B (Alama 70) Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. (a) Wanafunzi wa mkondo wa biashara wa shule ya secondari mikengo walitakiwa kufanya utafiti kwa njia ya mtandao ili kubaini shughuli mbalimbali zilizofanywa na makundi ya jamii ya asili ya kitanzania unadhani ni shughuli zipi walizibaini na kuzinukuu katika madaftari yao [taja nukta 5]

   (b) Taja sababu tano [5] za jamii ya asili ya Tanzania kuhama kutoka sehemu moja kwenda sehemu myingine

3. Tanzania ina takribani makabila mia moja na ishirini na kila kabila lina utamaduni wake wa asili pamoja na mila na desturi zake . Taja makabila manne makuu yanayopatikana Tanzania, na utaje asili ya kila kabila.

4. Watanzania wengi katika jamii ya leo tumetokana na wabantu kwani lugha nyingi za makabila nchini Tanzania hufanana matamshi pia hata maana. Eleza kwa kutoa mifano mitano (05) shughuli za kiuchumi na kijamii za jamii za Kibantu.

5. (a) Jamii yoyote isiyo na maadili inakuwa ni jamii mfuu . Maaadili katika jamii zetu yanachangia sehemu kubwa ya maendeleo ya watu na taifa zetu [taja nukta tano]

   (b) Bainisha matendo matano [5] ya kimaadili unayotenda au kutendewa na wenzako shuleni

6. Elia anataka kujua ipi ni tofauti kati ya Tekinolojia ya zama za mawe za kale na zama za chuma.

7. Uhusiano kati ya jamii za kitanzania na jamii za kigeni hasa ulaya ulipelekea athari mbalimbali kiuchumi, kisiasa na kijamii. Bainisha athari hizo kwa kutoa hoja tano

8. Mfumo wa kisiasa na kiuchumi katika kukuza maadili kwa jamii za kitanzania kuli kuwa na michango mingi. Kwa kutumia mifano toa hoja tano.

9. Shirika la umoja wa mataifa la sayansi, Elimu na utamaduni (UNESCO) linahitaji mwanafunzi atambue umuhimu wa urithi wa kihistoria katika jamii za kitanzania. Kwa kutumia mifano toa hoja tano kueleza umuhimu wa urithi huo

**SEHEMU C (Alama 15)**

**Jibu swali namba 10**

10. Shule ya Sekondari ‘’KATWE’’ kulikua na mgongano baina ya wanafunzi wa kidato cha kwanza ‘’a’’ wakidai kwamba somo la historia ya Tanzania na maadili halina faida kwao huku kidato cha kwanza ‘’b’’ hawajui somo linahusu nini kabisa. Wewe ukiwa kama mtaalamu wa historia na maswala ya utamaduni wasaidie wanafunzi wa kidato cha kwanza ‘’a’’ na ‘’b’’ katika shule ya ‘’KATWE’’ kujua umuhimu wa somo hilo.